ACMS
ADVENTIST CHURCH MANAGEMENT SYSTEM

# Mwongozo kwa Karani wa Kanisa Mahalia

@Musa Mandele

# YALIYOMO NDANI YA MWONGOZO


1. UTANGULIZI ..... 2
2. **KUINGIA KWENYE MFUMO** ..... 2
3. **SHUGHULI ZA USHIRIKA KATIKA MFUMO** ..... 3
   - 3.1. **Kusajili Mshiriki Mpya** ..... 3
   - 3.2. **Kutafuta** ..... 6
   - 3.3. **Kubadili baadhi ya taarifa za Mshiriki** ..... 8
   - 3.4. **Kumfuta/Kumuondoa** ..... 9
   - 3.5. **Uhamisho** ..... 10
   - 3.6. **Wasiojulikana walipo** ..... 12
   - 3.7. **Jina Kujirudia mara kadhaa** ..... 13
4. **Usimamizi wa Kanisa** ..... 14
5. **Maofisa wa Kanisa** ..... 14

## 1. UTANGULIZI

Toleo hili la mwongozo linahusika sana na shughuli za karani wa kanisa mahali hasa zile anazozifanya kwa kupitia mfumo wa ACMS. Utakapokuwa katika kujifunza yale yaliyoandikwa humu ndani, utagundua Kamba kuna maelezo ya ziada yatakayokuwa yakitolewa kwa njia ya picha ya kile kitakachoonekana katika komputa yako, baadhi ya picha hizi hazitakuwa na maelezo lakini jaribu kuzitumia na uone matokeo ya kufanya hivyo yako namna gani. Jaribu kwenda katika sehemu ya Reports na uone nini kinatokea au unaweza kufanya ukiwa kama karani katika mfumo huu wa ACMS.

Ikiwa utahitaji msaada wa karibu zaidi kuhusu ACMS, tafadhali wasiliana na viongozi wa ACMS waliowekwa kwa ngazi ya kila kanda. Kama hupati msaada wowote au hujui kiongozi wako ni nani, tafadhali sana tuma ujumbe wa barua pepe kupitia: acms@sncadventist.or.tz kwa msaada Zaidi au tuma ujumbe WhatsApp kwa namba +255620305729 na +255 754 353 736.

## 2. KUINGIA KWENYE MFUMO WA ACMS

Timu ya IT's na kamati ya mawasiliano toka conferensi ndiyo wanauwezo wa kukupa uwezo kama karani wa kanisa mahalia kuingia kwenye mfumo wa ACMS wataanza kukutengenezea akaunti yako (watakufanyia usajili). Hivyo makalani wa kanisa wanapaswa kutuma taarifa zao ikiwa ni Majina kamili, kanisa lako mtaa wako, barua pepe (E-mail) namba ya simu mwaka wako wa kuzaliwa ndipo Utapokea ujumbe kwa njia ya barua pepe uliyowapatia wasajili wako; kutakuwa na ujumbe unaokuelekeza kuisajili akaunti yako na unapokuwa umemaliza kuisajili akaunti yako,au utapewa username na password zako na utatakiwa kutembelea tovuti hii: www.acmsnet.org ili uingie kwenye mfumo. ZINGAZIA: unapoingia tu kwenye ACMS, unaweza ukajikuta uko kwenye uwanja wa kuanza kufanya kazi moja kwa moja, kabla ya hapo kiongozi wako anapaswa kwanza akupatie uwezekano wa kuweza kushughulika na kazi za ushirika wa kanisa.

Utakapotembelea tovuti iliyoandikwa hapo juu, utakuta sehemu imeandikwa **Sign in to Use ACMS**, Ingiza username na password kisha bofya

palipoandikwa **Sign In**: hakikisha ukurasa unao upata unalinganga na hayo maneno ili kuepuka kuingia mifumo mingine inayofanana na huu ili kuepuka usumbufu.




1: username inaweza kuwa email address yako au ile uliyotengenezewa mfano   mandelem au ina weza ikawa barua pepe yako mandelemusa@gmail.com

2: password ni ile utakayo kuwa umepewa zingatia  "case sensitivity" kama ilikuwa herufi kubwa basi hakikisha unaiweka kumbuka kuwa **nyanza2020** iko tofauti na **Nyanza2020** na iko tofauti na **Nyanza 2020**

3: kitufe kinakuwezeza kuingia kwenye mfumo

**VITU MUHIMU UKIINGIA KWA MARA YA KWANZA KWENYE   MFUMO UNAVYO TAKIWA KUVICHUNGUZA**

1: Majina yako

2: Kanisa na mtaa wako

3: Habari za jumla ambopo hapa inakupa idadi ya washiriki wako, taarifa za uhamisho na ripoti nyingine nyingi.


| ACMS | 1.675.0
acmsnet.org/Dashboard
ACMS
Musa Nathan Mandele
Home
Member
Church
Departments
Tools
Reports
Welcome!
The apostle Paul admonishes us to dress ourselves "in modest apparel, with pro- priety and moderation, not with braided hair or gold or pearls or costly clothing" (1 Tim. 2:9).
General information
467
Active members
0
Member entries in the year
0
Changes requested by Member
Transfers
1
0
Pending Transfers In (waiting on our side)
1
Pending Transfers Out (waiting on our side)
Whereabouts unknown
0
Whereabouts unknown
0
Whereabouts unknown no longer locked
Category
121
Attends regularly
2
Does not attend regularly
22
Attends In another SDA
322
No data
Acmsnet.org is an Official System of the Seventh-day Adventist Church · Privacy Policy · Version 1.675.0
District: Kiseke - SNYC
Church: Kiseke

# 3. SHUGHULI ZA USHIRIKA KATIKA MFUMO

Mfumo wa ACMS umetengenezwa ili kusaidia kazi ya usimamizi wa Ushirika wa Waadventita Wasabato katika kanisa mahalia. Shughuli zote za ushirika zinapatikana mahali palipoandikwa **Member**:




Ongeza mshiriki mpya kwa kubofya mahali palipoandikwa **Search/New** chini ya kimshale kwenye neno lililoandikwa **Member**:


| ACMS | 1.675.0
acmsnet.org/Dashboard
ACMS
Musa Nathan Mandele
Home
Member
Church
Departments
Tools
Reports
Search/New
Batch update
Transfer
Transfer (BETA)
Absent/Whereabouts unknown
Categories
ves "in modest apparel, with pro- priety and moderation, not with braided hair or gold or pearls or costly clothing" (1 Tim. 2:9).
General information
467
Active members
0
Member entries in the year
0
Changes requested by Member
Transfers
1
0
Pending Transfers In (waiting on our side)
1
Pending Transfers Out (waiting on our side)
Whereabouts unknown
0
Whereabouts unknown
0
Whereabouts unknown no longer locked
Category
121
Attends regularly
2
Does not attend regularly
22
Attends In another SDA
322
No data
Acmsnet.org is an Official System of the Seventh-day Adventist Church · Privacy Policy · Version 1.675.0
District: Kiseke - SNYC
Church: Kiseke
https://www.acmsnet.org/Membership/Member

Kisha, bofya mahalipalipoandikwa **New Member** upande wa kulia - juu wa screen yako:






**Taarifa Za Msingi Unapoongeza Mshiriki Mpya.**

Unaposajili mshiriki mpya taarifa za muhimu kuwa nazo ni Majina Yake (Kama yalivyo katika kitabu cha ushirika), Tarehe ya Kuzaliwa, Jinsia na taarifa za Mawasiliano.

Kama mshiriki huyu mpya anaingia kanisani kwako kwa njia ya ubatizo **"Baptism"** au kubatizwa tena **"Rebaptism"** hakikisha una tarehe ya ubatizo (Date of ceremony) na tarehe alipopitishwa kwa kura kuwa mshiriki wa kanisa (Date), Jina la Mchungaji aliyembatiza na mahali alipobatiziwa kwa usahihi.

Endapo itatokea kuwa mshiriki huyu alibatizwa zamani au aliingia kanisani kwako kwa kuhamisha ushirika zamani na hauna baadhi ya taarifa hizi kwa usahihi basi inashauriwa kuwa umuingize kama mshirika anaehamishwa "Adjustment".

Hata hivyo, kabla ya kusajili mshiriki tunatakiwa kuhakikisha kwamba bado hajasajiliwa na hivyo basi bofya mahali palipoandikwa Search. Kama mshiriki huyu amesajiliwa kama mshiriki wa kanisa jingine, jina lake na taarifa zake zitaonekana, la sivyo hakuna kitakachoonekana kumuhusu, ndipo utaendelea na hatua nyingine.

Sehemu iliyoandikwa **No phonetic search** itausaidia mfumo kufanya kazi ya kutafuta kwa haraka zaidi, hasa pale unapotafuta jina ambalo unauhakika na jinsi mpangilio wa herufi zake ulivyo bila kukosea herufi kubwa au ndogo. Hii inaweza kuwa njia rahisi zaidi ya kutafuta majina ambayo yana herufi za kawaida. Mfano; hapa chini tunalitafuta jina la Annah Mandele.




Baada ya kubofya **Search**, orodha itaonesha majina yanayokaribiana na jina unalolitafuta. Kama jina limeonekana utapaswa kufanya uchunguzi zaidi, ongea na huyo mshiriki, au mchungaji au ofisi za konferensi ili upate ushauri wa jinsi ya kufanya maana huyo mtu tayari ni mshiriki. Kama mshiriki hakuonekana katika orosha baada ya kumtafuta, bofya mahali palipoandikwa **Not Found**:




Baada ya kubofya **Not Found**, Program itafungua fomu ambayo inahitaji, Anuani, Mawasiliano, Taarifa nyingine zaidi na Taarifa zinazohusu ushirika wake msajiliwa. Kwa habari ya Taarifa kumhusu mshiriki Jina lake linahitaji, Jina la ukoo/la tatu linahitajika, Jinsia inatakiwa kufahamika, Tarehe ya kuzaliwa, Nchi aliyozaliwa na jinsi alivyofanyika kuwa mshiriki (taarifa hizi ni muhimu ili usajili kufanyaka). Hata hivyo jaza taaifa zote kwa kadri inavyowezekana maana taarifa nyingi zaidi zitarahisisha zaidi huduma za ACMS.


Search/New | ACMS | 1.675.0
acmsnet.org/Membership/Member
Home
Member
Church
Departments
Tools
Reports
Member
Search/New
Musa Nathan Mandele
Help ?
First Name
Last name
Birth Date (Optional)
Mother's Name (Optional)
Atupelye
Ambonhye
Search by first or last name
As is (no phonetic search)
Search
Ceremony
Type
Date
Ceremony/baptism date
Minute Number
Special Minute Number
Baptism
3/10/2023
3/10/2023
SNC/001/2023
SNC/01/03/2023
Place
Baptized by
First Bible Instructor
Second Bible Instructor
Kiseke
Personal data
Image
Code
First Name
Last name
Full Name
Atupelye
Ambonhwe
Atupelye Ambonhwe
Gender
Birth Date
Birth Country
Birth place
Male
3/10/2000
Tanzania
Mother's Name
Father's Name
Upload image
Known as
Acmsnet.org is an Official System of the Seventh-day Adventist Church
Privacy Policy
Version 1.675.0
District: Kiseke - SNYC
Church: Kiseke




Baada ya kujaza taarifa zote bofya **Save** na kisha ikiwa hukusahau baadhi ya taarifa ya muhimu utaona ujumbe unaosema **Success** ujumbe huu utakuwa upande wa juu wa screen yako ya komputa na utakuja juu ya mstari mpana wa kijani. Kama ukija ujumbe unaosema error fanya marekebisho na kisha bofya mahali palipoandikwa **Save** ili uone kama marekebisho yote yamefanyika na imeleta ijumbe wa Success.

**ZINGATIA:** Waulize viongozi wa ACMS katika kanda yako kuhusu namna ya kuwaunganisha watu pamoja hasa wale wa familia moja.

## 3.2. Kutafuta




Mara nyingi utakuwa unamtafuta mshiriki hai katika kanisa lako mahalia. Hata hivyo, ikiwa utaondoa alama ya vema/tiki kwenye kiboksi kilichoandikwa Local, jina litatafutwa katika orodha zote ulizoruhusiwa kuzisimamia au kuzitazama, na kama ukiondoa alama ya vema/tiki kwenye kiboksi kilichoandikwa Active, program itatafuta watu ambao walikwisha kuondolewa ushirika wao.

***KUMBUKA: Katika baadhi ya Konferensi na Misheni mshiriki hahesabiki kuwa washiriki mpaka wapitishwa na konferensi husika. Ikiwa konferensi yako inautaratibu huo hakikisha unawasiliana na katibu wako wa konferensi ili awarushusu watu hao kuonekana kama washiriki hai.***

Katika kutafuta jina mtu anaweza kuandika jina kamili au sehemu ya jina. Kwa mfano, "John Magembe", mtu anaweza kuandika "John" au akaandika "%Magembe". Katika mfano wa mwisho alama hii ya % inamaanisha "*sijui jina la kwanza ila jina la mwisho ni* ...................................... "




**NOTE: Ili uipate orodha yote ya washiriki wako wa kanisa mahalia, usiingize jina lolote. Bofya tu mahali palipoandikwa Search,** hapo ndipo majina yote ya washiriki wako yataonekana. Mfano huu hapa chini unaonesha majina yote saba ya washiriki wa kanisa letu la mfano, na katika orodha kama hii unaweza kubofya kichwa cha habari katika jedwali ili kuonesha mpangiilio wa majina kulingana na taarifa unayohitaji.


Search/New | ACMS | 1.675.0
acmsnet.org/Membership/Member
ACMS
Musa Nathan Mandele
Home Member Church Departments Tools Reports
Member
Search/New
Help ?
Search Member Interests
+ New Member
+ New Interest
More options
Person type
Select
PR MEM
Name/Code/Email
Search by first or last name
Local
As is (no phonetic search)
Ignore accents
Search
467 Records
Type Code First Name Last Name Birth Date Mother's Name Church Entity
MEM 10463187 Abel Hamis Hamis 7/14/1967 CHAUSIKU Kiseke SNYC - NTAU
MEM 10376326 Abia Kasiri Lulinga 1/1/1942 Nyasula Kiseke SNYC - NTAU
MEM 11147745 Abigaili Steven Magaso 2/2/1992 Eliada Kiseke SNYC - NTAU
MEM 10435128 Advenant Alfred 3/26/1994 VERYNICE Kiseke SNYC - NTAU
MEM 10380265 Agnes Deonatus Mang'oma 1/1/1968 Mhoja Kiseke SNYC - NTAU
MEM 10463157 Agnes Makuke Makuke 1/1/1972 MARTHA Kiseke SNYC - NTAU
MEM 9901031 Agness Maduhu Sanungu 11/10/1993 Habi Kiseke SNYC - NTAU
MEM 10830532 Albert Salvatory Kamalamo 4/19/1977 Astera Kiseke SNYC - NTAU
MEM 10827725 ALEX REUBEN MAKENE 2/17/2003 PENDO Kiseke SNYC - NTAU
Acmsnet.org is an Official System of the Seventh-day Adventist Church · Privacy Policy · Version 1.675.0
District: Kiseke - SNYC
Church: Kiseke

## 3.3. Kubadilisha baadhi ya Taarifa ya Mshiriki

Unapopokea baadhi ya mabadiliko yanayomuhusu mshiriki wako, kwa mfano mabadiliko ya anuani ya barua pepe, au unataka kuweka picha yake ambayo hapo kwanza hukuiweka unaweza kufanya hivyo kwa kubofya mahali penye kialama cha kalamu kama hiki hapa: alama hii iko kando tu kidogo na jina la muhusika unayetaka kubadilishia taarifa zake. Ingaza taarifa unazotaka kubadilisha na kisha bofya mahali palipoandikwa Save.




*Dondoo: Ili kuwatia moyo washiriki kuleta taarifa zinazohitajika, tengeneza "fomu ya usajili" kwa ajili ya kanisa lako na uitawanye kwa kila mshiriki na uwaombe wairejeshe wakiwa wana maoni na wakiwa wameijaza. Fomu hii utaipata mahali hapa kwenye mfumo:* ***Reports ▯Member ▯Member Reports ▯Registration Form.***

## 3.4. Kuondoa /Kufuta Ushirika

Ikiwa mtu amelala mauti, au kanisa limepigia kura kuondolewa kwa ushirika wake au kwaamba hakulikani alipo bofya alama hii ⇄ (Alama hii inaitwa Transaction Button) kando tu ya jina lake katika orodha ya washiriki mahali penye dots 3:




Baada ya kubofya kitajitokeza kijidirisha kingine chenye muhtasari wa taarifa za muhimu zinazomuhusu muhusika na itakupatia ruhusa ya kuchagua kufanya mojawapo kati ya haya mambo manne:




**Death** – Bofya hapo ikiwa mtu amelala mauti, unapobofya mahali hapo program itamletea karani wa kanisa kuandika tarehe ya kifo cha mshiriki.

**Censure and Removal** **(Makaripio & Kufuta Ushirika)** – Bofya hapa kulingana na maelekezo yanayotolewa katika Sura ya 7 ya mwongozo wa Mwongozo wa Kanisa la Waadventista Wasabato.

**Missing** – Sehemu hii itamruhusu karani kutekeleza kile ambacho mwongozo wa kanisa unasema katika sura ya 6 na ya 7 kuhusiana na watu wasiojulikana walipo (Angalia katika Kipengele cha 3.6 kwa maelezo zaidi kuhusiana na hili).

## 3.5. Uhamisho

Hatua za uhamisho zitaanza mara tu mshiriki anapokuwa amehamia kanisa jingine na kuongea na karani wake wa kanisa. Wewe kama karani unayempokea mshiriki huyo, nenda sehemu iliyoandikwa **Member** na kisha bofya mahali palipoandikwa Transfer. Baada ya hapo bofya mahali palipoandikwa **Transferring to our church** na hapo utakuwa umeanza hatua za kuuleta ushirika wake kanisani kwako.




Hapo mahali palipoandikwa **Transferring to our church**,ingiza jina la kanisa mahali ulipo ushirika wa huyu anayehama kwa wakati huo, andika pia jina lake na kisha bofya mahali palipoandikwa **Search**:



Bofya upande wa kushoto wa jina husika (itatokea alama ya vema/tiki) kisha bofya mahali palipoandikwa **Include** na hapo utakuwa umetuma ombi la kuomba ushirika wa muhusika kutoka kwa kanisa lake mahalia. Tazama kielelezo chake hapa:




Kanisa linalopaswa kutuma jina la ushirika litapokea ujumbe wa ombi la uhamisho wa ushirika na watatakiwa kupitisha kuhama kwa jina hilo. Wao watakwenda kwenye mtandao wa ACMS na kuofya sehemu iliyoandikwa **Transferring out of our church**. watabofya sehemu ya ombi la uhamisho wa mshiriki, wataingiza tarehe na namba ya ajenda ya kupitisha ushirika wake na ndipo watabofya neno **Send**.

Kwa upande wa kanisa lako, yaani kanisa linalopokea ushirika, mtapokea ujumbe kwamba mshiriki ameruhusiwa kuhamisha ushirika kuja kanisani kwako na sasa mtapaswa kumpigia kura ya kumpokea kama mshiriki. Ile sehemu ya **Transferring to our church** itaonesha maombi yote ya uhamisho ambayo yako tayari kukubaliwa yakiwa na ujumbe huu: **Sent/Granted**. Baada ya kanisa kupiga kura ya kumpokwa, bofya kiboksi kushoto mwa jina la muhusika (itatokea alama ya vema/tiki) ingiza tarehe ya kura na namba ya agenda na kisha bofya **Accept**:


Transfer | ACMS | 1.675.0
acmsnet.org/Membership/Transfer
Church search
Mabatini
Name | Type | Entity | City | State | Country
Mabatini | Church | South Nyanza Conference - Northern Tanzania Union Conference | Select
Mabatini | Church | Western Tanzania Conference - Northern Tanzania Union Conference | Biharamulo | Kagera | Tanzania | Select
Mabatini | Company | Western Kenya Conference - West Kenya Union Conference | Bungoma | Kenya | Select
Mabatini-isandula | Church | South Nyanza Conference - Northern Tanzania Union Conference | Select
Transfer status
Pre-request
Request
Waiting for Conference/Union
Sending
Search
0 Records




Utakuja ujumbe ulioandikwa **Success** utaonekana katika komputa yako ikiwa mshiriki amefanikiwa kuhama. Kama umepata ujumbe unaoonesha Error, fuata maelekezo au wasiliana na wataalam wa ACMS ili upate msaada zaidi.



**KUMBUKA:** Makanisa yenye ACMS ndiyo yatakayofanikiwa kutumia program hii. Ikiwa kanisa lako halijasajiliwa katika mfumo huu wa ACMS tafadhali wasiliana na wahusika wa ACMS katika eneo lako ili kupata utaratibu wa uhamisho uliopo.

## 3.6. Wasiojulikana walipo

ACMS inaweza kusaidia kwa habari ya wale wasiojulikana mahali walipo. Kwa kuwaruhusu makarani kuonesha orosha ya wale wasiojulikana walipo, makarani wengine wanaweza kuonesha mahali muhusika alipo. Ili kulifanya hili Nenda kwenye New kisha nenda kwenye **Absent Member** kisha muweke mtu katika orodha ya watu wasiojulikana walipo.




Ili kumuweka mtu katika orodha ya watu wasiojulikana walipo bofya mahali palipoandikwa **Add to Absent Member List**, andika jina la mshiriki na kisha bofya **Search**:




Ingiza tarehe kanisa lako mlipoanza kumtafuta mshiriki huyu rasmi (Inaweza ikawa ni tarehe hii ambayo unashughulika na kumtafuta katika ACMS au tarehe flani hapo kabla). Mwongozo wa kanisa unashauri kwamba mtu muhusika aanze kutafutwa miaka miwili kabla ya kuondolewa kwa jina lake ktk ushirika.

Nenda kwenye jina unalolitafuta na kisha bofya **Include**. ***Hata kama kanisa lako wamekuwa wakimtafuta mtu huyo kwa miaka miwili sasa, bado ACMS itaendelea kuhitaji mtu huyo atafutwe tena angalau kwa siku zingine 90.*** Bofya kiboksi kushoto mwa jina husika na utaona alama ya vema/tiki

kisha bofya **Include**.


Absent/Whereabouts unknown |
acmsnet.org/Membership/Missing
Nathan Mandele
Home Member
Member
Search
Full Name
Birth Date
Mother's Name
mandele
As is (no phonetic search)
Search
Help ?
2 Records
Results
Full Name | Birth Date | Mother's name | Church | Entity
Joyce Mussa Mandele | 10/23/1991 | happy | Kiseke | South Nyanza Conference | Northern Tanzania Union Conference
Musa Nathan Mandele | 8/18/1987 | Anyuvise | Kiseke | South Nyanza Conference | Northern Tanzania Union Conference
Started
3/10/2023
Include
Close
Search
Entity
Kiseke
0 Records
District: Kiseke - SNYC
Church: Kiseke

Baadhi ya makanisa katika Konferensi yako, wanaoweza kusaidia kumtafuta/kumpata mtu huyo, wanaweza kutoa taarifa kwa kupitia mwishoni kabisa mwa jina la mtu anayetafutwa. Ikiwa jina husika lina maandishi yaliyokolezwa, maana yake mtu flani ameandika taarifa flani kumuhusu anayetafutwa. Ili kuiona taarifa hiyo bofya palepale kwenye kile kialama cha kwanza.

Ikiwa unataka kulifuta jina kutoka orodha ya wanaotafutwa, bofya mbele kidogo tu baada ya jina husika.




Ikiwa jina la muhusika limetafutwa kwa miaka miwili na hajapatikana (Tangu tarehe rasmi ilipowekwa ili kumtafuta),na tayari muhusika amewekwa kwenye orodha ya wasiojulikana walipo katika ACMS kwa siku

90, kanisa lako mahalia wanaweza kupiga kura ya wale wasiojulikana walipo, mnaweza kupiga kura ya kutokujulikana alipo. Mara tu baada ya kulipigia kura, bofya katika kiboksi kushoto kidogo tu, kabala ya jina lake ya jina lake. Ingiza Tarehe ya mliyopiga kura kwenye "transaction date" na namba ya ajenda kwenye "minute number" na kisha bofya mahali palipoandikwa “Update”:




*Kumbuka: Njia nyignine ya kuwaweka watu katika orodha ya Wasiojulikana walipo "Absent Member List" ni kubofya alama hii mara tu baada ya*

*jina lake katika orodha ya majina ya washiriki au baada ya kulitafuta na kisha bofya sehemu iliyoandikwa "Missing" kama inavyooneshwa katika Sehemu3.4.*

## 3.7. Majina Yanayojirudia mara Kadhaa

Ikiwa umegundua kwamba kanisa lako limeingiza taarifa za mtu mmoja mara mbili katika ACMS Wasiliana na viongozi wako wa ACMS nao watalitazama tatizo na kukushauri juu ya njia bora zaidi ya kuliondoa tatizo hilo. Usijisikie vibaya kutoa taarifa wala pasiwe na ugumu katika kufanya hivyo kwani ni heri kutoa taarifa kuliko kuwa na ushirika wa mtu mmoja mara mbili.




Duplicate Members | ACMS | 1.6
acmsnet.org/Membership/MemberDuplicatedReport
Musa Nathan Mandele
Home
Member
Church
Departments
Tools
Reports
Member
Duplicate Members
Items Compared
Full Name - Birth Date - Birth place - Mother's name - Baptism date - Baptismal pastor
Options
Minimum level of comparison
2
Person type
Select
PR
MEM
Only check person types selected
List/Print
Export to Excel
Acmsnet.org is an Official System of the Seventh-day Adventist Church · Privacy Policy · Version 1.675.0
District: Kiseke - SNYC
Church: Kiseke


Duplicate Members | ACMS | 1.6
10ed7e79-8200-429b-92d8-b90
blob:https://www.acmsnet.org/10ed7e79-8200-429b-92d8-b90749e08b99
10ed7e79-8200-429b-92d8-b90749e08b99
2 / 4
181%
1
2
3
4
Frola Lucas 2 January 1
Frola Lucas 2 January 1
Jacklin Pastory 2 January 1
Jacklin Pastory 2 1/1/2000 1/1/0001
Jackson Thomas 2 1/1/2000 1/1/0001
Jackson Thomas 2 1/1/2000 1/1/0001
Joshua Lucas 2 January 1
Joshua Lucas 2 1/1/2000 1/1/0001
Joshua Lucas 2 1/1/2000 1/1/0001
Joyce Jackson 2 1/1/2000 1/1/0001
Joyce Jackson 2 January 1
Joyce Jackson 2 January 1
Joyce Jackson 2 January 1
Leah Yohana 2 1/1/2000 1/1/0001
Leah Yohana 2 January 1
Leah Yohana 2 January 1
Magreth Richard 2 January 1


Search/New | ACMS | 1.675.0
acmsnet.org/Membership/Member
ACMS
Musa Nathan Mandele
Home
Member
Church
Departments
Tools
Reports
Member
Search/New
Help ?
Search
Member
Interests
New Member
New Interest
More options
Person type
Name/Code/Email
Select
joshua lucas
Local
As is (no phonetic search)
Ignore accents
Search
PR
MEM
2 Records
Type
Code
First Name
Last Name
Birth Date
Mother's Name
Church
Entity
MEM 16243328 Joshua Lucas 1/1/2000 Kiseke SNYC - NTAU
MEM 16243320 Joshua Lucas 1/1/2000 Kiseke SNYC - NTAU
Acmsnet.org is an Official System of the Seventh-day Adventist Church · Privacy Policy · Version 1.675.0
District: Kiseke - SNYC
Church: Kiseke


Search/New | ACMS | 1.675.0
acmsnet.org/Membership/Member
ACMS
Musa Nathan Mandele
Home
Member
Church
Departments
Tools
Reports
Member
Search/New
Help ?
Search
Member
Interests
New Member
New Interest
More options
Person type
Name/Code/Email
Select
joshua lucas
Local
As is (no phonetic search)
Ignore accents
PR
MEM
2 Records
Baptism form 0
Change to
Transaction
Roles 0
Merge records
New user
Type
Code
First Name
Last Name
Birth Date
Mother's Name
Church
Entity
MEM 16243328 Joshua Lucas 1/1/2000 Kiseke SNYC - NTAU
MEM 16243320 Joshua Lucas 1/1/2000 Kiseke SNYC - NTAU
Acmsnet.org is an Official System of the Seventh-day Adventist Church · Privacy Policy · Version 1.675.0
District: Kiseke - SNYC
Church: Kiseke


Search/New | ACMS | 1.675.0
acmsnet.org/Membership/Member
Merge records
Transactions | Primary - Joshua Lucas
Date
Transaction
Church
External church
1/1/2000
Adjustment
Kiseke
Undone Transaction
Awaiting Approval
Secondary
Name/Code/Email
Birth Date (Optional)
Mother's Name (Optional)
joshua lucas
Search by first or last name
As is (no phonetic search)
Search
1 Records
Type
Code
First Name
Last Name
Mother's Name
Church
Entity
MEM
16243328
Joshua
Lucas
Kiseke
South Nyanza Conference | Northern Tanzania Union Conference
Select
Merge
Close

# 4. SHUGHULI ZA KANISA

Ilii kutazama na kupata taarifa zinazohusiana na anuani za kanisa jingine, au kuongeza taarifa flani kuhusiana na kanisa lako, nenda kwenye sehemu iliyoandikwa **Church** :




Ingiza jina la kanisa, au sehemu ya jina la kanisa, chagua au acha sehemu zenye viboksi vya kufanyia mchujo wa kile unachotafuta na kisha bofya **Search**. Bofya kialama cha Edit chenye mwonekano wa kalamu na kisha jaza taarifa unazohitaji kulihusu kanisa lako au kanisa jingine:







Ukurasa unaohusika ana taarifa za kanisa utakupatia fursa ya kuona au kuweka picha ya kanisa, mtaa, anuani, taarifa za mawasiliano, muda wa huduma na mengine zaidi.

## 5. Maofisa wa Kanisa

Tunapokuwa na orodha kamili ya viongozi wa kanisa ni rahisi kuwabaini katika mtandao wa ACMS. Nenda sehemu iliyoandikwa **Departments** kisha bofya **Church Officers:**




Ili kumuweka mtu katika orodha ya viongozi bofya **New** mahali flani juu upande wa kulia penye alama ya +


Church Officers | ACMS | 1.675.0
acmsnet.org/RoleMember
Musa Nathan Mandele
Home Member Church Departments Tools Reports
Departments
Church Officers
Help ?
Search Officer
New officer
Department
Role
Started
Expires On
Secretariat
Select
3/10/2023
3/10/2024
Evangelism
Family Ministries
Health Ministries
Home and School Association
Interests Coordinator
Internet Ministries
Junior/Teen Ministries
Leadership Club
Men's Ministries
Music
Pathfinder Club
Patrimonial
Personal Ministries
Possibilities Ministry
Public Affairs and Religious Liberty
Public Evangelism Coordinator
Publishing Ministries
Sabbath School
School Board
Secretariat
Search
District: Kiseke - SNYC
Church: Kiseke


Church Officers | ACMS | 1.675.0
acmsnet.org/RoleMember
Musa Nathan Mandele
Home Member Church Departments Tools Reports
Departments
Church Officers
Help ?
Search Officer
New officer
Department
Role
Started
Expires On
Secretariat
Select
3/10/2023
3/10/2024
Didn't find the department? create a new one here
Member
Select
Data protection coordinator
Designated Safeguarding Person
Disclosure Clerk
District Secretary, Coordinating
District Secretary, Editing
Health and Safety Officer
Membership consultant
Secretary/Clerk
Secretary/Clerk, Associate
Secretary/Clerk, Minutes
District: Kiseke - SNYC
Church: Kiseke

Ingiza sehemu au jina lake kamili kisha bofya mahali palipoandikwa **Search**:




Katika orodha ya majina yaliyoonekana, bofya **Select** mbele ya jina unalotaka:

Ingiza tarehe (tarehe anayoanza kazi) na tarehe anayotazamiwa kuachia uongozi (unaweza pia kuiacha tarehe hii bila kujaza kama haitaleta shida), chagua idara yake, na pia boya mahali penye box la **ACMS Access.** Hapo utakuwa umewapatia uwezekano wa kuitumia ACMS kwa mambo yanayowahusu, baada ya hapo bofya **Save**:

***Bwana awabariki mnapoendelea kufanyia mazoezi features mbalimbali za ACMS ili kujijengea uwezo zaidi kwenye mfumo huu.***